TANGAZO LA SERIKALI NA. 234 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 814 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya jumla

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa-
(a) kufuta maneno "kifungu cha" popote yanapoonekana na badala yake kuweka maneno "kanuni ya"; na
(b) kufuta maneno "kifungu kidogo cha" popote yanapoonekana na badala yake kuweka maneno "kanuni ndogo ya".

Marekebisho ya kanuni ya 3

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "madini ya ujenzi" kama ifuatavyo:

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa au madini mengine yanayotumika katika ujenzi;".

Marekebisho ya kanuni ya 5

4. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwakatika kanuni ya 5 kwa kufuta na kuandika upya maneno ya utangulizi kama ifuatavyo:

> "Mtu, taasisi au kampuni iliyowasilisha maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini na kukubaliwa itapaswa-".

Marekebisho ya kanuni ya 10

5. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 10 kwa kuongeza kanuni ndogo ifuatayo mara baada ya kanuni ndogo ya (4):

> "(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (4), adhabu ya kufutwa au kusimamishwa kwa kibali itadumu kwa muda wa mwezi mmoja tangu ilipotolewa na baada ya kuisha kwa muda huo utaratibu wa kuomba kibali upya utapaswa kufuatwa.".

Marekebisho ya kanuni ya 12

6. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 12 kwa kubadili mpangilio wa aya (f) kuwa maneno ya kufungia.

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*